



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO KATIKA  
JIMBO LA MUHAMBEWE**

**Dodoma, Machi 27, 2021.**

Kama tunavyofahamu, Taifa letu liko kwenye kipindi cha maombolezo kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Tume inatoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Familia ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Chama cha Mapinduzi na watanzania wote kwa ujumla.

Pamoja na kuendelea na kipindi cha maombolezo ya kitaifa, Tume inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Kwa muktadha huo, Tume ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ameitaarifu Tume **uwepo wa nafasi wazi ya kiti cha Ubunge katika Jimbo la Muhambe**, Halmashauri ya wilaya ya Kibondo, Mkoani Kigoma kuanzia tarehe 12 Februari, 2021, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mhandisi Atashasta Nditiye.

Aidha, kwa kuzingatia kifungu cha 37 (1) (b), cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343 ambacho kinaitaka Tume kujaza nafasi ya kiti cha Ubunge katika kipindi kisichopungua siku 20 na kisichozidi siku 50 tangu kutokea kwa sababu iliyoacha nafasi wazi ya kiti hicho.


Kutokana na matakwa hayo ya kisheria, Tume inautaarifu Umma kuwa Jimbo la Muhambe liko wazi na uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 3 Aprili, 2021 ambayo ni siku ya 49 tangu kutokea kwa kifo hicho. Hivyo, uchaguzi utafanyika kwa ratiba ifuatayo:-

Na.	Tukio	Tarehe
1.	<b>Kutoa Fomu za Uteuzi</b>	<b>28 Machi – 03 Aprili, 2021</b>
2.	<b>Uteuzi wa Wagombea</b>	<b>03 Aprili, 2021</b>

3.	<b>Kampeni za Uchaguzi</b>	<b>04 Aprili – 01 Mei, 2021</b>
4.	<b>Siku ya Uchaguzi</b>	<b>02 Mei, 2021</b>

Tume tayari imekwisha vitaarifu Vyama vya Siasa kwa njia ya barua juu ya kuwepo kwa uchaguzi huo mdogo na inavikumbusha kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Miongozo na Maelekezo ya Tume wakati wote wa kipindi cha Uchaguzi.

Imetolewa na:

  
 Dkt. Wilson Mahera Charles  
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**